# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI 102/1
# MTIHANI WA PAMOJA WA TARAFA YA KABONDO – 2015

1 **Ni insha ya tahariri**

Iwe na anwani

Utangulizi - Mwanafunzi ataje/aeleze alikotoa habari

**Mwili** - Mwanafunzi azingatie hoja hizi.

a) Sababu au chanzo cha ukosefu wa usalama au mauaji.

.Siassa-Vyama vya kisiasa

.Uchochezi kutoka kwa viongozi.

.Chuki na uhasama baina ya makabila

.Umaskini

.Ukosefu wa ajira

.Ugaidi

.Dhuluma za kihistoria.

.Vikundi haramu vya vijana kama vile Mungiki,Sungusungu na Alshabab.

**Hitimisho/Mapendekezo:**

.Mtahiniwa atoe njia mwafaka za kukabiliana na utovu wa usalama Nchini.

Wachochezi kuchukuliwa hatua za kisheria.

.Wananchi kuhamazishwa kuhusu umuhimu wa kuishi pamoja kwa amani.

.Serikali na washikadau kushirikiana ili kukabili tatizo la umaskini.

.Kubuni nafasi za ajira kwa vijana.

.Serikali kukabili vikundi haramu na ugaidi.

**Tarbihi** -Mapendekezo ya tokana na sababu za hapo juu.

**Mtahiniwa** -Ahitimize kwa kuandika jina Lake

Sahihi

Mahali anakotoka.

www.eeducationgroup.com

3 Mkono usioweza kuukata ubusu.

Ni insha ya methali;

Mwanafunzi abuni kisa kinachoeleza matumizi ya methali.

Methali hii hutumiwa kushauri watu kuwa hapana haja ya kushindana na watu wanaotuzidi nguvu,madaraka au uwezo.

4 Ni insha ya mdokezo

.Sharti mwanafunzi amalize kwa maneno aliyopewa.

.Kisha kieleze hali ambapo mtu alinusurika kifo akiwa timboni aidha kwa kuporomokewa mchanga au kuvamiwa kama ilivyo kuwa Mandera ambapo wachimba migodi walivamiwa usiku wa manane na kundi la Alshabab na akapatikan miongoni mwa wafu

# MTIHANI WA WA KABONDO MWONGOZO WA KISWAHILI KARATASI LA TATU

1 A USHAIRI

a) Chema hakidumu

b)i) Ukaraguni-vina vya ukwapi na utao vinavyo badilika badilika katika beni zote

ii) Utenzi-kwa jumla,mistari ni ya urefu wa mizani kumi na mbili tu.

iii) Ukara-ubeti wa kwanza na wa pili tu-kina cha ukwapi kinabadilika bali cha utao hakibadiliki.

iv) Kikwamba-neno chema limeanza beti zote

2 x2 =4 za kwanza 2

Kutaya alama 1

Maelezo 1

c) Umbo la beti mbili za mwisho

i) Kila ubeti una mishororo mine

ii) Kila mishororo una vipande viwili-ukwapi na utao.

iii) Mistari ina urefu wa mizani kumi na mbili -6a , 6b

iv) Kila msitari una vina viwachi vya kat na vya kati na vya mwisho.

v) Vina vya kati na vya mwisho vinabadilikabadilika katika ubeti wan ne na tano.

-bu-e
-bu-e } ubeti wa nne
-bu-e

-ni-ngu } ubeti wa tano
-ni-ngu

zote 4 x 1 = 4

d) Toni ya shairi hili ni mayonzi/huzuni/maombolezo nafsi nani poteza wapendwa wake wlooaga. Yoyote 1 x 2 = 2

e) Dhamira ya wahenga katika shairi hili ni kuonyesha machungu mtu anapitia anapopoteza wapendwa wake kwa kifo au

-kuonyesha kuwa vitu vizuri na haridumu. 1 x 2 = 2

f) Mbinu ya inkisari

n’ongeza-ninaongeza

Alijipa-aliyejipa 2x2=4

Lazima ataje mfano na kuandika kwa njia ya kawaida

g) i) Kinashanilisha-kimeshaniliza/kimenifanyanilie.

ii) ela-ila/isipokuwa/bali 1x2=2

SEHEMU B: RIWAYA

Kidagaa

2 a) -mnenyi ni mwalimu majisifu

-anamwambia mkewe Dora

-wako nyumbani mwake

-dora anachukizwa na tabia ya majisifu ya kulewa chakari na kumwachia majukumu ya kuwalea wale watoto mapacha walemavu/Dora analalamika kuwa majisifu hamsaidi kuwalea wale watoto wao walemavu bali kazi ya ni kulewa tu.

4x1=4

b) i) ushaji/tashihishi/huishi-unaniamsha damu

ii) maswali balagha-wataka mimi nipike?/Enhee? Wewe unaniamsha damu?

iii) kuchanganya ndimi/ndimi mseto-bloody blastered

zote mbili za kwanza 2x2=4

kutaja alama 1

mfano alama 1

c) mnenaji ni mwalimu majisifu

maadhui yanayoendelezwa na majisifu ni

i) ulevi-majisifu ni mlevi wa kupindukia

ii) ndoa-hawajibiki katika ndoa-anaonyesha ndoa zilizo na matatizo hasa kwa kutowajika kwa wanaume katika ndoa

iii) wizi-aliuiba mswada wa arusi na kuubadilisha kuwa yake

iv) uzembe wa watumishi wa serikali-majisifu hakuwa anahudhuria vipindi vyake darasani kama ilivyotarajiwa.

v) ulaghai/wonge/tama-ametumiwa kuendeleza maudhui haya kwa vile

alikuwa na tama ya kulimbikiziwa sifa anapoitwa wangwani kitoa mhadhara ilhali hakuwa mwandishi wa kidagaa.pia ana tama ya kujifaidi kutokana na mswada wa amani

vi) ubabe-dume/taasubi ya kiume-anaeleza haya kwa vile hakufuata mashauri ya mkewe bali alimnyanyasa kwa kumlimbikizia majukumu yote ya kuwalea wanao walemavu.

vii) ukatili-alidhulumu wanawe aliwaita mashata kumlenga bibi

zozote 6x2=12

mwanafunzi asitaje sifa za mhusika kama vile mlevi,mwizi,mzembe nk.

viii) mabadiliko-kumwomba mke amani.imani,msamaha na kuwapenda wanawe

ix) unafiki-kudai aliibiwa nakala zake.

x) mgogoro-kati yake nasaba na bibiye

3 Anwani kidagaa kimemwozea ni jazanda

Kidaga ni samaki wadogo ambao hawaozi kwa urahisi badala ya kukaushwa imetika kijazanda kuonyesha kuaribika kwa jambo/kuenda mrama hasa kwa kuhusika katika riwaya mifano

i) kidaga kimwemwozea imani kwao Baraka baada ya nyumba ya kushonwa na mamake kuuwawa.

ii) kidaga kimemwozea imani anaponyanganywa mswada wake na majisifu.

iii) kidaga kimemwozea Bab Dj kaptura yake inapoliwa na fahali kando yam to kiberenge

iv) kidaga kimemwozea mwalimu majisifu anaposhindwa kutoa mhadhara wangwau

v) kidaga kimemwozea amani anapolazimizwa kuyalea kitoto uhuru ambaye anawatia

vi) mtemi nasaba bora bintiye mashaka anapomwasi na kukataa kujilinga kazi jeshini

vii) mashaka anapokea barua ya ben maozi ya kutamatisha urafiki kati yao.

viii) amani anapopatikana kwa nasaba bora usiku anapigwa nusura auwawe na mtemi.

ix) amani/imani na matuko weye wanatiwa jela kwa makosa yasiyokuwepo(kuzingiziwa tu.

x) amani kufukuzwa chuoni bbaada ya wanafunzi kuweka karatasi za uchochezi katika chumba chake chuoni.

xi) mtemi nasaba bora anajitia kitanzi wa kutoa uhai wake. Zozote 10x2=20

lazima wahusika watajwe majina.

4 SEHEMU C HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI

a)

i) haya ni maneno ya mhadhiri mzungu na wanafunzi kupitia kwa mwandishi

ii) yameelekezwa kwa fikirini

iii) yanayoonyesha jinsi waafrika wlivyodhalilishwa na wazungu nchini marekani

iv) fikirini anakumbuka/anawaza alipojikuta darasani yeye peke yake mweusi

4x1=4

b) mbinu ya lugha ni;

swali balagha-je kule kwenu watu wanavaa nguo au wanatembea rabana

kutaja 1

mfano 1

jumla 2

c) masaibu saba yanayowakumba waafrika ughaibuni kwa mujibu wa hadithi damu nyeusi

-kuachwa na dereva mzungu katika kituo cha kuabiri magari ya abiria

-mama mzungu kuwaita polisi kwa kuwa hakuwa amefunga zipu ya suruali yake alipotoka hotelini.

-kutuhi miwa na kufuatwa na bawabu kuwa mchopozi alipokwenda dukani.

-fiona kumdanganya kuwa anampeleka chuoni kumbe alitaka kumpora

-fiona alitaka kumnajisi na kumuua

-bob na Fiona kumpora vitu vyake vyote na kumtupa nje uchi siku ya barafu

-kuulizwa na bob ni nini kinamtoa kwao afrika na kuja kuwakera huko marekani,kuwa waafrika kuhusishwa na uchawi.

-kutozwa faini mara mbili kwa kuvuka barabara taa zikiwa nyekundu ilhali wazungu hawashikwi.

-alijikuta kisiwa kimoja katika bahari ya wanafunzi weupe.

-kubaguliwa na wahadhiri wazungu kwa kupendelea katika alama na shahada chuoni

-kuulizwa maswali ya kumdhalilisha na wenzake chuoni n.k.

Zozote saba za kwanza 7x2=14

5 a) Matumizi ya ishara katika hadithi ya gilasi ya mwisho makaburini

i) msoi aliamka kwa moyo mzito na shingo upande alipopitiwa na semkwa waende kwenye baa yao maarufu.

ii) msoi kuangusha bakuli lake la maua baada ya kujikwa mlangoni

iii) mbingu ilikasirika njia gghafla-ikafunga uso wake mweusi

iv msoi alikaa akitazama mavani kinyume na jinsi alivyopenda kukaa akiipa mgongo

v) msoi hakuwa na furaha yoyote na kumjibu asha mwezi na nyota zimeshuka kidogo kuja kuikaribisha msiba wetu"

vi) taa siku hiyo zilikuwa na mwako wa huzuni,ingawa zilikuwa zinapiganisha rangi kama kawaida.

vii) mlango wa gari kumfinya msoi vidole.

viii) msoi alipojitosa kucheza na asha,hakuonyesha usogora wake wa kila siku.

Zozote 5x2=10

b) Matatizo yanayokumba asasi ya ndoa katika hadidhi

i) mke wangu

kutoelewana kutokana na

-utabaka

-elimu

-utamaduni

-falsafa (alama 5)

ii) mwana wa darubini

-ukware

-ulevi

-ukatili

-unafiki

-malezi mabaya k.m mwakitawa.

-kifo

6 a)

i) ni nje ya ofisi ya meya

ii) ni sauti za wafanyakazi wa barabara la cheneo

iii) meya yuko ofisini mwake ndiye anayeelezwa sauti hizi

iv) wafanyakazi wa barabara la cheneo wamefika kumlalamikia meya kuhusu haki zao zilizopuuzwa 4x1=4

b)

i) elimu duni-meya anawapeleka wanawe ng'ambo

ii) ukosefu wa chakula-mama anamlisha mtoto chakula kilichoharibika.

iii) ukosefu wa dawa hospitalini

iv) mshahara duni/kuchelewa kulipwa

v) ufisa-unyakuzi wa ardhi-meja/bili

vi) propaganda-dawa zimegizwa ilhali hazifiki.

vii) ukosefu wa maji cheneo isipokuwa kwa meya.

viii) maliwani kulipa kodi ilhali wnanchi wenye mapato duni kama muuza mboga anatozwa kodi

ix) gharama ya maisha kupanda-mamakes dararu hawezi kumudu gharama ya mafuta na makaa.

x) ukosefu wa nafasi za kazi-vijana waliohitimu kutoka vyuo vikuu ni wengi ingawa hawana kazi

xi) kupigwa kwa wafanyakazi wa baraza la cheneo na askari wanapogoma kudai haki zao.

xii) ukosefu wa vifaa vya kazi-glaru zozote 5x2=10
lazima mtahiniwa ataje wahusika.

c

i) migomo-wafanyikazi wa bara la cheneo waligoma kuonyesha kutoridhika na hali ya kazi,malipo duni

ii) kujiuzulu kwa wafanyakazi-warudi

iii) vyama vya wafanyakazi-tatu,medi,beka

iv) mashauriano na meya-siki zozote 3x2=6

7 i) upuuzaji wa haki za wanafunzi
ii) ubadhirifu
iii) dhuluma
iv) umaskini
v) utabaka
vi) tamaa
vii) ubinafsi
viii) huduma mbovu kwa umma
ix) unafiki/uwongo wa viongozi

8 a) maagizo ni utanzu wa fasihi simulizi wenye tungo
Zenye mpangilio wa maneno na ambazo huhusisha watu wanaaotenda au kugiza mbele ya watu wanaotazama(hadhira)
Ni sanaa ya maonyesho inayojumulisha kusema na kutenda kama afanyayo mtu au kiumbe mwingine(igiza) mbele ya hadhira. Yoyote 1x2=2

b) i) kuwepo kwa hadhira ambayo hutazama maigizo
ii) kuwepo kwa wahusika wanaoigiza
iii) kuwepo kwa mahali (jukwa)
iv) kuwepo kwa mavazi yanayohusishwa na wahusika
maleba na malebo zozote 4x2=8

c) ngomezi ni matumizi ya ngoma au ala badala ya maneno kuwasilisha ujumbe.1x2=2

d) Sifa za ngomezi
i) kuwepo kwa ngoma
ii) mapigo ya ngoma yafuate toni na mizani au ridhimu ambayo huwasilisha maneno Fulani
iii) wasikilizaji wa ngoma au ujumbe ambao unawasilishwa na maneno hayo.
iv) kueleweka kwa mapigo hayo na jamii.mapigo ya ngoma huwakilisha maneno Fulani kiasi kwamba wanajamii wanaweza kujua kunasemwa ni nini kwa kuyasikiliza tu.
v) kuwapo kwa ala nyingine. 4x2=8

e) i) Shughuli:zinazohusishwa na miviga

-jando/tohara

-kutawazwa kwa kiongozi

-mavuno

-Kuzaliwa kwa motto/motto kupewa jina

-mazishi

-ndoa

-urithi wa mke n.k.

ii) Hasara za miviga katika jamii ya leo

-baadhi ya miviga zimepitwa na wakati k.v tohara ya wasichana.

-zingine ni gharama k.v mazishi na ndoa.

-zingine zina athari ya kiafya k.v urithi wa wanawake enzi hizi za ukimwi.